

HUDUMA YA KWANZA
KWA NDOA ILIYOATHIRIKA

Na: Marilin Phillipps

Copyright © 2010
ISBN

Kimechapwa 2010

**Eden Publishing Company inakutia moyo kugawa nakala ya kitabu hiki kwa ye yote anayekihitaji.
Ingawa, si ruhusa kunukuu sehemu yo yote ya kitabu hiki kwa ajili ya kuuza.**

Mistari yote ya Biblia imenukuliwa kutoka katika The Holy Bible in Kiswahili, Union Version
Published as Biblia Maandiko Matakatifu © 1997 Bible Society of Tanzania, P.O Box 175, Dodoma,
Tanzania.

DIBAJI

Mume wangu, Mikaeli pamoja nami, ndoa yetu imeponywa na nguvu za Yesu Kristo. Ni miaka michache tu iliyopita tulikuwa tumefikia hatua ya kupeana talaka. Mikaeli alikuwa akifanya mipango ya kuo mke mwingine. Washauri hawakuonesha tumaini hata kidogo, mchungaji wetu alikuwa amekata tamaa na kufikia uamuzi kuwa ndoa yetu ilikuwa imekufa kabisa, na baadhi ya Wakristo wenzangu walinishauri nichukue vilivyo vyangu niondoke na kuanza maisha mapya.

Kipindi hiki cha ugomvi kilifanyika kuwa ni kipindi cha mafunzo maishani mwangu maana nilijifunza uthabiti na kuzitegemea nguvu za Bwana. Neno la Mungu likidhiihirika ndani yako, Mungu yuko tayari kulithibitisha kwa uwezo na nguvu. Neno haliwezi kusema, "mtu asivunje" ndoa kama hakuna nguvu ya Mungu iwezayo kurejesha na kuiponya ndoa ile. Roho Mtakatifu aliniongoza hatua kwa hatua katika kuiponya ndoa yetu na Yesu akathibitisha tena kuwa hakuna lisilowezekana kwake. Ndoa yetu iliponywa kwa nguvu za Mungu na mamlaka ya Neno lake.

Madhumuni ya kitabu hiki siyo kuzama ndani sana katika mafundisho ya kusimama kwa ajili ya uponyaji wa ndoa yako. Kimekusudiwa kama jina la kitabu livilyo, Huduma ya kwanza, kwa maumivu ya mwanzo yanayojitokeza katika ndoa yenu. Utatakiwa utafute msaada kutoka kwa mchungaji wako pamoja na Wakristo wengine ili kupata msimamo ulio mzuri. Pia kuna makundi mbalimbali ambayo yameitwa na Mungu yanayoweza kukusaidia katika nyakati kama hizi.

Kitabu hiki kimeandika kwa ajili yako. Usikate tamaa. Usichoke katika kutenda mema. Tambua kuwa Mungu huwajali watu. Kile alichotutendea sisi, anataka awatendee na ninyi pia.

Katika Jina la Yesu,

Marilin Phillipps

UTANGULIZI

Ni miaka michache tu iliyopita, mtu aliyefahamu ni nini kilichokuwa kikitendeka katika ndoa yetu, hasa yule aliyenifahamu kuwa nilikuwa mume wa namna gani, asingeota kuwa siku moja nitaandika utangulizi wa kitabu cha uponyaji wa ndoa. Mawazo yangu yalikuwa yamejiandaa kuachana na mzigo huu wa ndoa. Nilijiona kuwa nimebeba mzigo wa watoto wawili na mwininge alikuwa karibu kuzaliwa. Nilishikwa na tamaa na kumpenda mwanamke (rafiki wa karibu wa mke wangu) "aliyenifahamu" napenda nini. Pia nilishikwa na tamaa ya pesa. Akili zangu zilitumikishwa kwa kutazama picha za uchi pamoja na ulevi. Nilijithamini peke yangu, na kujawa na ubinafsi. Sikumjali Mungu bali nilijiona kuwa mimi ninajitoshereza kwa kutimiza matakwa ya mwili wangu.

Hebu mwone mtu yule anayeelezwa katika 2 Timotheo 3:2-5. "*Maana watu watakuwa wakujipenda wenye, wenyenye kupenda fedha, wenyenye kujisifu, wenyenye kiburi, wenyenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi. Wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenyenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenyenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao jiepusha nao.*" Maelezo hayo yananielezea jinsi nilivyokuwa.

Lakini... Atukuzwe Bwana kwamba tuna Mungu ambaye ni Mungu wa IMANI. Atukuzwe Mungu kwamba wale wanaomtumikia wanaweza kuwa nayo imani yake. Wanaweza kuona kwa macho ya kiroho na si kwa macho ya kimwili. Maono yake kwangu (na watu wote) yalikuwa ya tofauti kabisa na jinsi nilivyokuwa. Mungu alinitaka niwe mtu wake, kwa tabia iliyoolezwa katika Neno lake. 1 Timotheo 3:2-4 inazungumza juu ya mtu wa Mungu ambaye "...asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mtu wa kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu." Kwa nyongeza alimtaka mke wangu, aliyekuwa katika agano la mahusiano naye, pamoja nami tuwe katika uhusiano ule ambao Adamu na Hawa walikuwa nao kabla ya anguko, ni uhusiano ule unaozungumzwa katika Yeremia 32:38-41, kwamba ndoa yetu iwe ya moyo mmoja na njia moja ili tuweze kubarikiwa na Mungu ili tuweze kuzaa matunda katika ulimwengu huu.

Inaonekana kuwa ingekuwa rahisi kwa mke wangu kuyatazama matukio na vituko vyote vilivyokuwa vikijitokeza. Inaonekana ingekuwa rahisi kwake kujilinda nafsi yake kwa kujijali yeye mwenye. Lakini hiyo siyo njia ya Mungu. Kitu halisi alichokisema Mungu kwake ni kwamba kama atajiachilia kwa Mungu na neno lake, hapatakuwa na cho chote kile kitakachomzuia kuzipokea baraka zote za agano zilizoahidiwa katika neno lake.

Ndivyo alivyofanya. Alijiachilia kwa Mungu na Neno lake kwa kutokufanya mambo kwa njia za kidunia. Kwa muda wa miaka mitatu yenye machungu, akitiwa moyo na watu wachache tu ndani ya jamii ya Wakristo, na hakuna hata moja kutoka kwangu, alisimama na kuvipiga vita akiyatufuta mapenzi ya Bwana maishani mwake. Havikuwa vita virahisi; kuna wakati alikata tamaa, lakini alikuwa na moyo wa kumtafuta Mungu. Kitabu hiki kitakuonesha sehemu ya ile vita unayoipiga. Lakini yeye aliye ndani yetu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu. Ushindi ni wako. Mshindi husongwa na maangamizi. Katika mfano wa ushindi wa mke wangu, sasa ana mume (ambaye ni mimi) ambaye anamtumikia Bwana na kukua katika ndoa ambayo inaleta heshima katika huduma ya Mungu.

Usemi wangu huu unaweza kusikika kama ni wa ajabu, lakini naomba uelewewe. Mke wangu alikuwa na wakati mgumu sana LAKINI alistahili. Alistahili, ndoa yetu ilistahili. Usimruhusu yule mwovu aibe, anyang'anye na kuiua ndoa yenu. Wewe na mwenzi wako mna kusudi la kitauba kwa ajili ya ndoa yenu, ili iwe siraha yenye nguvu wakati huu wa sasa pamoja na majeraha yake, bali utazameni moyo wa Mungu pamoja na maono yake juu ya ndoa yenu, "*kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyombayo au tuyawazayo*" (Efe. 3:20).

Mikaeli Phillips

Marilin, nakupenda na ahsante sana kwa kusimama imara wakati wa matukio magumu ya kuiponya ndoa yetu.

YALIYOMO

Sura ya I	1
Sura ya II	4
Sura ya III	7
Sura ya IV	9
Sura ya V	12
Sura ya VI	15

Mshtuko

Siku ya kwanza kabisa Mikaeli aliponijulisha kwamba amepata mwingine zaidi, na anmpango wa kunipa talaka, nilishtuka. Ghafla, akili zangu ziliganda na hisia pia. Nilihisi kufa.

Nilikuwa nimegundua kuwa mambo yalikuwa yameharibika kati yetu, lakini mara kwa mara niliwaza kwamba mambo hayo tutayashughulikia na kufikia kikomo. Zaidi ya yote, sisi tunapendana. Tumeoana. Kesho mambo yatakuwa mazuri tu.

Punde si punde, maana mambo yalikuwa yakiendelea kuwa magumu tu, mume wangu aliondoka na wala hakutaka kufanya cho chote kile cha kuinusrus ndoa yetu. Alitamka kuwa hanipendi na wala hajawahi kunipenda. Kipindi hiki nilikuwa na ujauzito wa tatu, nilihisi kusalitiwa na kuonewa. Nakumbuka siku moja jioni nikiwa nimekaa bafuni nililia kwa nguvu sana nikahisi mwili wangu kufa. Kila kitu kilikuwa giza na bila tumaini.

Mikaeli hakutaka ushauri wa aina yo yote. Hakutaka kuzungumza nami. Alichokitaka ni tendo la ndoa tu. Nilijihisi mpweke na mtu asiyefaa kabisa. Ushauri wa "marafiki" zangu haukunisaidia maana wao waliniambia niachane nao, waache wafurahie maisha pamoja.

Nilikwenda kwa mchungaji na kuniambia kuwa hakuna cha zaidi kinachoweza kufanyika. Aliniambia kwamba ilikuwa hali ya kusikitisha na ninapaswa nikubaliane na hali halisi. Hatimaye Mikaeli alitafuta mshauri baada ya kuambiwa kwamba hiyo itamsaidia akifika mahakamani kwa ajili ya kumbukumbu. Baada ya kuongea na mshauri huyu kwa mara ya kwanza yeye alishauri tupeane talaka haraka iwezekanavyo ili kuokoa muda pamoja na fedha. Alisema tulikuwa tumefikia hatua mbaya mno ambayo haina msaada.

Kisha nilikwenda kwa rafiki yangu ambaye nilifahamu anamtumikia Mungu kwa nguvu. Kama kuna mtu anayejua Biblia inasema nini, yeye anaweza. Aliniambia kuwa Mungu anaweza kuiheshimu talaka hiyo kwa kuwa Mikaeli amejiingiza katika uzinzi. Aliniambia kwamba haoni kitu ambacho kingeweza kusaidia kama Mikaeli hayuko tayari kuonesha ushirikiano.

Hatimaye nikaenda kwa Yesu. Inachekesha kuona jinsi gani inavyotuchukua muda mrefu kufika pale ambapo tulipaswa kufika mara ya kwanza tu shida inapotokea.

Yesu alikutana nami katikati ya maumivu na machozi yangu. Alinifaraji, alinipenda na kuanza kunipa msimamo wa uhakika. Alinionesha waziwazi kutoka katika neno lake ile misingi ya ndoa. Aliziondoa hisia zangu na kunifundisha iliyo kweli.

Hili ndilo kusudi la kitabu hiki – KWELI. Kama unataka huruma na machozi, utayapata maana yako tayari tayari. Watu watalia nawe na kukulilia kwa urahisi sana. Kama unataka kujihesabia haki kwa kutokusamehewa kwao, hiyo nayo utaipata pia. Wapo wengi walioumizwa, hivyo watakuwa upande wako wakati wa maumivu. Kama unataka ukweli ulio wazi na rahisi, neno la Mungu litakupatia. Ni ngumu kuuchukua kwa mara ya kwanza, lakini Yesu ameuahidi, "*tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru*" (Yohana 8:32).

Kuna nguvu katika hiyo kweli. Kuna uponyaji katika hiyo kweli. Kuna kuhuishwa katika hiyo kweli. Sasa tambua hili, dakika hii, **YESU ANATAKA NDOA YAKO IPONE**.

Kama unasoma kitabu hiki ninakisia kuwa ndoa yako inashida. Yawezekana umeshashikwa na mshtuko. Hukutegemea kama yote haya yangekupata. Hukuamini kama inawezekana. Unahitaji msaada.

Kwanza kabisa, hakuna njia ya mzunguko – unamhitaji Yesu. Kama unatarajia ndoa yako ipone kwa njia nyiningezo mbali na nguvu yake, umepotoka. Pasipo Yesu, ndoa inaweza kugundishwa pamoja. Daima kutakuwa na makosa ambayo yataendelea kuleta mgandamizo. Yesu pekee ndiye

anayeweza kuponya ndoa hata yale majeraha ya zamani yasioneokane. Ukweli ni kwamba ukiwa na Yesu kile kilichokidhaifu hutiwa nguvu. Hakuna makosa yatakayobaki kuendelea kukuletea mgandamizo.

Yesu anakupenda. Hivyo ulivyo. Huhitaji kusafishwa kwa ajili yake ili akupokee. Huhitaji kuwa mwema au kujikusanya pointi ili umkaribie. Yeye alikufa kwa ajili yako ulipokuwa ungali mwenye dhambi. Anakujuva vema kuliko mtu mwingine awaye yote, hata zaidi ya vile unavyojitambua wewe. Huwezi kumdanganya. Anaujuva moyo wako.

Sasa hivi unapaswa umgeukia na kujitoa kwake. Ni yeye peke yake awezaye kukusafisha dhambi zako na kuyanyosha maisha yako. Huwezi kufanya wewe mwenyewe. Kama utachukua hatua hutakuwa tena katika shida uliyonayo sasa. Ni yeye peke yake anayeweza kuitengeneza ndoa yako. Omba sala hii na mpe Yesu moyo wako.

“Yesu ninaumia. Nimekataliwa na ninajisikia sina thamani kabisa. Nimejithidi kurekebisha mambo kwa juhusi zangu mwenyewe nimeshindwa. Nimechoka kutoa udhuru, nimechoka kujaribu. Ninakiri mbele zako ya kuwa mimi ni mwenye dhambi. Siwezi kujisafisha mwenyewe na siwezi kuyatengeneza maisha yangu mimi mwenyewe. Ninayatoa maisha yangu kwako, Yesu. Ninakupokea wewe uwe mwokozi na Bwana wa maisha yangu. Ninaupokea utakaso wako wa damu kwa ajili ya dhambi zangu. Ninakupa maisha yangu uyatawale sasa hivi. Nisaidie, Bwana. Nifariji. Nifundishe. Ninakuhitaji zaidi maishani mwangu. Baba, Mimi ni mwanaao.”

Kama umeomba sala hii kwa kumaanisha kile ulichokuwa ukikisema, wewe sasa umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Hii ina maanisha kwamba ile asili ya kale, ile uliyozaliwa nayo, imerithiwa na asili mpya, asili ya Mungu. Utaihitaji asili hii wakati wa kusimama kwa ajili ya uponyaji wa ndoa yako. Huwezi kufanya kwa nguvu zako mwenyewe. Lazima ufanye kwa nguvu zake.

Mungu ameandika barua maalum juu ya upendo kwa ajili ya watoto wake. Inaelezea kila nyanja katika maisha haya hapa duniani, na kwa kila hali. Katika barua yake ya upendo, Mungu ameyaeleza mapenzi yake na kuonesha ni kwa jinsi gani unaweza kuyapata. Barua yake ya upendo ni Biblia.

Yawezekana hapo awali umejaribu kusoma Biblia na ikaonekana kwako kama unasoma Kiyunani. Hali hiyo ipo kwa sababu ulikuwa unasoma barua ya mtu mwingine. Sasa wewe umezaliwa upya, ni mtoto wa Mungu na barua umeandikiwa wewe. Kwa sasa utailewa maana umeandikiwa wewe na Roho wake akaaye ndani yako atakufundisha yote. Kama ndiyo mara yako ya kwanza kumwamini Yesu, kuna mambo mengi ambayo unapaswa ujifunze. Usichoke na kukata tamaa. Mungu anajua wewe ni mgeni katika jambo hili. Yeye atakuongoza kwa upole.

Hata kama umemjua Mungu kwa muda mrefu sasa, utakuwa na kazi ya kufanya mbele yako. Uko vitani daima kwa ajili ya nyumba na familia yako. Hii ni kazi. Hii siyo kazi ya kutendewa bali ni kazi ya kutenda mwenyewe. Utakwenda kujifunza maana ya kuwa askari ndani ya jeshi la Bwana. Haya ni mashambulizi ya ana kwa ana, bali atukuzwe Mungu maana amewawezesha watoto wake kuvipiga vita vizuri.

Unapaswa kutambua kwamba adui yako, Shetani, na majeshi yake wanatamani kuiangamiza nyumba yenu. Wanatumia matukio pamoja na watu. Ni muhimu kutambua:

WATU SIO ADUI ZAKO.

MATUKIO SIO TATIZO.

USISHIKE TAMA.

Shetani ni bingwa wa matukio. Usijaribu kuzitumia siraha zake ukitegemea kushinda vita. Ukifanya madai yenyе misingi ya matukio ("Usipoachana na tabia hiyo, mimi nitaondoka nikuache") atatumia matukio hayo kukudanganya ili utimize haja ya moyo wako. Kushika tama hujenga mazingira ya matukio ambayo matokeo yake si ya kitaufa. Kuna watu wengi wametalakana bila kukusudia, bali walijikuta wamejiweka katika hali hiyo kwa maneno ya vinywa vyao.

Shetani ana mchezo mbaya. Anajua ni nini kitakachokuumiza zaidi, hivyo huvitumia vitu hivyo ili akuumize hisia zako. Kwa sasa, yule umpendaye sana, mwenzi wako, anasema na kufanya mambo ya kutisha na kusikitisha sana. **MWENZI WAKO SI ADUI YAKO**. Kumbuka kwamba mwenzi wako anatumiwa na adui ili kuivunja nyumba yenu. Sijali kama mwenzi wako ni Mkristo na ana mistari mingi ya Bibila kichwani mwake anayoweza kuieleza ili kutetea yale anayoyafanya. **SI MPANGO WA MUNGU NDOA YENU KUVUNJIKA**.

Usijali watu wanasema nini. Je! Mungu anasema nini? Je! Biblia inasema nini?

Usijali watu wanafanya nini. Je! Mungu anafanya nini? Je! Biblia inasema nini juu ya yale unayopaswa kuyafanya?

Nyumba yako iko chini ya mashambulizi ya yule adui. Kama unataka kuyashinda mashambulizi ni lazima ukitambue kile kinachotokea sasa na jinsi ya kupambana nacho. Sura inayofuata itakusaidia sana.

"Yesu, ninatambua nyumba yetu iko chini ya mashambulizi ya yule adui. Ninahitaji msaada wako. Sijui namna ya kupambana ili nishinde. Sijui cha kufanya. Ninaikabidhi vita hii kwako. Nifundishe, nisaidie. Fanya, nitakuamini wewe. Amina."

Dalili

Kwa nini yote haya yanatukia? Kwa nini wewe? Kwa nini ndoa yako? Je! Umefanya nini au hujafanya nini mpaka kusababisha jambo hili?

Kuielewa migogoro ndani ya nyumba yenu, unapaswa kufahamu baadhi ya kanuni ambazo zinapatikana katika neno la Mungu, Biblia. Mungu alipomuumba mwanamume na mwanamke wa kwanza aliwaunganisha pamoja katika ndoa, uhusiano wa agano. Ili tuilewewe ndoa kama Mungu anavyoilewa, ni lazima tulielewe agano kama Mungu anavyoilewa.

Agano ni makubaliano kati ya watu wawili ambayo yanawaunganisha wote katika uhusiano wa ndani sana na tena ni wa kudumu. Hii inamaanisha kwamba si maisha ya wawili tena, bali wanashirikiana maisha ya aina moja. Katika Biblia tunamwona Mungu alifanya maagano na watu mbalimbali, agano linalokumbukwa sana ni lile alilolifanya na Ibrahim kwa kuanzisha taifa la Kiyahudi (Mwanzo 12:1-3). Kwa kifo na ufufuo wa Yesu Kristo, wote wanaompokea Bwana na Mwokozi ni washiriki wa Agano Jipyaa na Mungu (Waebrania 8:6-13).

Upendo wa agano una nguvu. Husema, “Ninautoa uhai wangu kwa ajili yako” (1 Wakorintho 13:1-8). Ndani ya Biblia tunamwona Mungu akibaki kuwa mwaminifu katika ahadi zake alizoziahidi hata kama mtu, mshiriki wa agano lake anaposhindwa kulitunza agano. Agano la upendo ni uaminifu bila kujali upande mwingine unafanya nini. Sababu ni kwamba katika kila agano kuna ahadi pamoja na masharti. Watu wanapoingia katika agano huahidiana mambo fulani kila mmoja kwa mwenzake na kuweka wazi masharti yatakayowasaidia kutunza agano lao. Kama mmoja hatakuwa mwaminifu katika ahadi zake, haimsababishi yule mwingine naye kutokuwa mwaminifu. Katika Agano la Kale tunamwona Mungu, mshika agano mwaminifu, akiwaita Israeli, mshirika asiyemwaminifu kwa agano. Ukengeufu wa Israeli haukumbadilisha Mungu na ahadi zake kwake. Anaendelea kumtetea, kumpenda, kumwita amrudie hata leo.

Biblia inaiita ndoa kuwa ni uhusiano wa agano. (“...angawa yeye ni mwenzako, na mke wa agano lako” Malaki 2:14). Ulipooa uliingia katika agano. Kama sehemu ya sherehe wakati wa arusi yenu, wewe na mwenzi wako mliahidiana mambo fulani fulani kila mmoja. Sentensi zinaweza kutofautiana kwa kila arusi, lakini maneno yanayoweza kujirudia-rudia ni kama vile “upendo, heshima, wa thamani, utii”, n.k. Katika sherehe yenu kulikuwa na masharti au viapo kama vile, “katika mema au mabaya, katika utajiri au umaskini, katika ugonjwa au uzima.” Yawezekana viapo hivyo viliambatana na maneno kama vile, “...hadi kifo kitakapotutenganisha.” Hivi huitwa viapo vyta arusi. Biblia inalo la kusema juu ya viapo. “Wewe ukimwekea Mungu nadhiri, usikawie kuiondoa; kwa kuwa yeye hawi radhi na wapumbavu; basi, uiondoe hiyo uliyoiveka nadhiri. Ni afadhali usiweke nadhiri, Kuliko kuiweka usiiondoe” Mhubiri 5:4,5.

Wengi wetu hatukujua maana ya viapo hivi wakati tulipofunga ndoa. Hisia zetu zilikuwa juu sana kiasi kwamba hatukujua ni nini hasa tunakisema. Lakini Mungu alikuwa akitusikiliza.

Ninakumbuka baada tu ya ndoa yetu kupona, rafiki yangu alinipongeza kwa kazi nzuri ambayo nilikuwa nimeifanya. Nilipokuwa nikimsikiliza, nilijisikia nakujiona wa ajabu kulingana na mateso niliyoyapata. Nilijisikia kuwa Mungu anafurahi kuwa mimi sasa ni sehemu ya timu yake. Hata hivyo, nilizidi kujuliza, kuna wengine wangapi ambao wamekuwa waaminifu kwa Neno lake. Nilipokuwa nikirudi nyumbani kutoka nyumbani kwake, Bwana alisema na moyo wangu, “Je! Ulifanya kitu gani katika kuvisimamia ndoa yenu ambacho hukukiahidi siku ya arusi yenu?

Ghafla, niligundua kwamba Mungu alikuwa akisikiliza siku ya arusi yetu, zamani hata kabla hatujamjua yeye, yeye alikuwa ametunza kumbukumbu ya maneno yote tuliyoyasema siku hiyo. Wakati wa “hata kwa mabaya” ulipokuja, yeye alibaki kuwa mwaminifu katika ndoa yetu na

kututarajia sisi pia. Inaonekana si kawaida siku hizi ambapo kuna ndoa na talaka za haraka haraka kuisimamia ndoa, bali kwa kufuata vigezo vya Mungu, hakuna jambo lisilo la kawaida

Katika sura iliyopita, nilidokeza kwamba hatuwezi kupata msaada wa kutosha kutoka kwa wachungaji au kutoka kwa washauri. Hata yule rafiki yetu aliyekuwa amezaliwa mara ya pili, amejazwa na roho, na anamatumikia Bwana, alitangaza kuwa ndoa yetu ilikuwa imekufa kwa sababu ya uzinzi. Bali Mungu ana vigezo tofauti. Nikiwa njiani narudi nyumbani baada ya kupokea ushauri wangu wa mwisho nilijitayarisha kupokea talaka jambo ambalo lilikuwa dhahiri mbele yangu. Upendo wangu wa kimwili kwa mume wangu ulikuwa umekufa kwa sababu ya majeraha ambayo nimekuwa nikiyapata. Niliwaza, kama kweli Mungu alijua ndoa hii kwamba imekufa na haipo na atanipatia mume mwingine, kwa nini asifanye hivyo ili niachane na msongamano wa matatizo haya.

Hata kama tukiwa tumempokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi, akiwa anatawala ndani, yeze husema na miyo yetu kupitia Neno lake. Sijawahi kuisikia sauti ya Mungu hadharani, lakini sina shida ya kutambua ni wakati gani anasema nami ndani yangu. Siku ile aliniongoza hadi kupata mstari wa Biblia ambao sikumbuki kama nilikuwa nimewahi kuusoma. “*Lakini wale waliokwesha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana; mke aseachane na mumewe; lakini, ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe*” (1 Wakorintho 7:10,11).

Niligadhabika nilipouona mstari huu. Sikuamini ni kwa nini Mungu anakuwa mgumu hivi katika swala hili. Punde si punde nilifungua Biblia na kuufikia mstari ambao nilikuwa nimepewa na yule rafiki yangu ambao ulinisaidia “nikubali” talaka na kuolewa tena. Nilimwonesha Mungu na kumwuliza yeze alifikiri nini. Kwa upole alinirejesha katika 1 Wakorintho 7:10,11 na kuniomba nisome tena. Polepole ilianza kuingia akilini mwangu kwamba Mungu hafanyi mzaha. Jambo hili ni la kuzingatia. Yeze ndiye aliziweka sheria hizo kwa hiyo alikuwa akizisistiza. Nilighafilika kidogo kwamba mbona hana kanuni zilezile kwa kila mmoja. Nilimweleza wazi juu ya Wakristo wengi ninaowafahamu ambao wametalakana na kisha kuoa au kuolewa tena, aliwaza nini juu yao. Kwa mara nyingine hakusema neno bali alinirejesha tena katika 1 Wakorintho 7:10, 11. Aliniambia, “Hiki ndicho kigezo changu. Una uhuru wa kuamua, nami nitakutana nawe katika uamuzi wo wote ule utakaoufanya. Ukiama kubaki peke yako, mimi nitakuwa mume wako. Nitawatunza watoto wako kama baba yao. Hutapungukiwa na kitu cho chote hata watoto pia. Nitakutunza zaidi ya mume wa kidunia. Kama utaamua kupatana na mwenzi wako, hata hivyo, nitakushindia.”

Ghafla nilikumbuka andiko hili, “*Usiogope; maana hutatahayarika; wala usifadhaike; maana hutaaibishwa; kwa kuwa utaisahau aibu ya ujana wako, pia mashutumu ya ujane wako hutayakumbuka tena. Kwa sababu Muumba wako ni mume wako; BWANA wa majeshi ndilo jina lake; na Mtakatifu wa Israeli ndiye Mkombozi wako; Yeye ataitwa Mungu wa dunia yote*” (Isaya 54:4-6) na “*Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane, Mungu katika kao lake takatifu*” (Zaburi 68:5). Nilitambua kuwa alimaanisha kile alichokuwa akisema.

Uamuzi haukunichukua muda mrefu. Sikutaka kuwa peke yangu. Nilikuwa na watoto wawili pamoja na ujauzito. Nilitaka kuwa na mume pamoja na mahali pa kuishi. Niliitaka ndoa yetu. Nilimwambia Bwana, “Bwana, ninataka kupatana na mume wangu, lakini sijui nifanye nini. Sijapata mtu wa kuniambia kuwa inawezekana.”

“Nasema inawezekana,” lilikuwa jibu lake. “Nitakufundisha namna ya kufanya.”

Ndoa yako ni uhusiano wa agano, picha ya hapa duniani kuonesha agano la upendo la Mungu wetu. Shetani hapendi umoja na nguvu ya agano na anatafuta kuangamiza ndoa zote anapweza kuzipata (Yohana 10:10). Kile ambacho umefanya au hujakifanya kinawenza kuchangia katika anguko la ndoa yako, lakini si sababu. Shetani na majeshi yake wamejipanga kuiangamiza ndoa yako. Mambo yote yanayotokea kwa sasa ni silaha zake tu za maangamizi. Jina la Yesu ni jina ambalo linayapita majina yote. Ni jina la tatizo gani ambalo unahangaika nalo kwa sasa? Uzinzi? Ulevi? Ndoa ya jinsia moja? Zinaa ya maharimu – baba kuzini na binti yake? Haijalishi ni jina gani tatizo lako linaitwa, jina hilo liko chini ya jina la Yesu. Maandiko yanasema kila kitu lazima kiliungamie jina la Yesu. “*Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe , la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba*” (Wafilipi 2:9-11).

MBINU KUU YA YULE MWOVU NI KUKUSHAWISHI KWAMBA TATIZO HILI NI KUBWA SANA NA MUNGU HALIWEZI. Huo ni uongo! Wewe uko katika agano na Mungu kuitia damu ya Yesu na wewe unasimamia uhusiano wa agano uliobarikiwa na Mungu hapa duniani. Je! Kuzimu ina nguvu kiasi gani dhidi ya hili?

Sasa wakati unasoma sentensi hiyo hapo juu, yule adui alikunong' ononeza, "Lakini inakuwaje kama ndoa hii haijabarikiwa na Mungu? Je! Inakuwaje kama Mungu hataki ipone? Labda halikuwa swala la '*Kile alichokiunganisha Mungu*'. Kama Mungu alikuwa ameukubali mpango huu, kwa nini uharibike kiasi hiki?"

Naomba ukumbuke ukweli huu, Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa. Mume na mke wanapoamua kuingia katika uhusiano wa ndoa, wanaingia katika mpango wa Mungu. Mara ndoa inapofungwa Mungu hujitoa kuhakikisha kwamba mpango huo unafanikiwa. "Kile Mungu alichokiunganisha" haiwahusu wale tu waliokubaliana kuoana. Hii ni njia nzuri sana, kuwa katikati ya mapenzi ya Mungu, lakini ni wachache sana wanaomtafuta Mungu wakati wa kutafuta mwenzi. Wenzi wengi, tukiwemo na sisi, tulioana kwa matakwa yetu na Mungu hakuhusika kwa lo lote. Ingawa, hii haibadilishi mwito wake wa agano la upendo na uaminifu. Ni mapenzi ya Mungu kwa kila mmoja kuwa katika agano naye na ndoa zote zimwelekee yeye. Hata kama hali halisi siyo hiyo, yeye yuko pamoja na wanandoa pamoja na ndoa 100%. Kuvunja ndoa ni tendo baya kama vile kutoa mimba eti kwa sababu mtoto huyo hakuwa amekusudiwa. Punde unapokuwa katika uhusiano wa agano, mwombe Mungu akufundishe jinsi ya kuuleta katika ukamilifu wake. Mungu ni mwaminifu kwao wote walioingia katika agano naye hata kama tukionesha hali ya kushindwa. Mungu anapenda tujifunze kuwa waaminifu kwake hata kama wenzi wetu hawataonesha uaminifu.

"Bwana Yesu, nifundishe kujua maana ya agano. Nifundishe kuwa imara na mwaminifu kwa maneno yangu hata kama mwenzi wangu siyo. Natamani niujue moyo wako juu ya agano. Nataka niione ndoa yetu kama uionavyo wewe. Yesu, pendo langu kwa sasa limevunjika-vunjika. Peke yangu siwezi. Kwa sasa sijisikii kupenda au kuutoa mwili wangu. Tafadhali, nisaidie Bwana. Nitapumzika kwako."

Maumivu

Kwa sasa una maumivu – maumivu makali kiasi kwamba hujui kama yatakwisha. Ninajua, maana mimi mwenyewe nimeyapitia hayo. Ngoja nikuhakikishie kwamba maumivu hayo yatakwisha. Yesu akiponya, huponya kweli kweli.

Siku moja nilipokuwa nikimwita Mungu katikati ya maumivu yangu, Yesu alinichukua na kunipeleka mpaka bustani ya Gethsemane (Marko 14:32-42). Kwa mara ya kwanza niliyaona mateso aliyoteseka huko. Muda na wakati ambao alihitaji faraja kutoka kwa mtu mwingine, wanafunzi wake walikuwa wamelala wote. Hawakuya elewa maumivu yake, hata hawakujali. Wao walikuwa wamekula mlo mzuri na sasa ilikuwa ni usiku walichohitaji ni usingizi.

Je! Unaojisikia kama vile hakuna mtu anayejua hisia zako kwa sasa? Je! Unaona kama hakuna mtu anayeyajua mateso yako kwa sasa? Yesu anajua. Yeye amekwisha kuhi upweke wako, kukataliwa kwako, na maumivu yako. Yeye ameyabeba yote ili wewe usiwe na mzigo wa kubeba. Yeye alikuwa katika maumivu makali kiasi kwamba hata machozi yake yaligeuka kuwa matone ya damu. Yeye hakupata faraja ili akufariji wewe. Mruhusu akufariji sasa. Zaburi 144 mstari 2 unasema kwamba Bwana ndiye "*mhisani wangu na boma langu, Ngome yangu na mwokozi wangu, Ngao yangu niliyemkabilia, Huwatiisha watu wangu chini yangu*". Mgeukie yeye sasa hivi. Mwache yeye afanyike mhisani, ngome, na ngao yako. Yeye anakupenda sana. Ni yeye peke yake anayefahamu ni kwa kiasi gani umeumia. Mruhusu akufariji.

Yesu alinionesha kitu kingine ambacho kilitokea pale bustanini. Alisalitiwa na mmoja wa wapendwa wake, alisalitiwa kwa jina la upendo, na busu (Mathayo 26:47-50). Yule unayempenda sana amekusaliti. Yesu anajua unachokihisi kwa sasa. Alidharauliwa na kuaibishwa. Yeye aliyabeba yote hayo ili wewe uwe huru. Alipogongomewa msalabani hakuchukua dhambi zako tu, bali aliyachukua maumivu yako yote, kudharauliwa na aibu yako, na kusalitiwa kwako. Waembrania 12:2,3 inasema "*tukimtzama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza amani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu , naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Maana mtafakarini sana yeye aliyeyastahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia miyoni mwenu.*"

Roho Mtakatifu alipomwongoza Paulo kuandika maneno hayo, alikuwa nawe mawazoni. Alijua maumivu utakayoyapata leo hii. Alijua aibu ya kukataliwa ambayo utaipata. Anakutaka umtazame Yesu. Maneno hayo yaliandikwa ili ujue cha kufanya saa mbaya inapokupata maishani.

Hata kabla ya kuanza kumwomba Yesu kuiponya ndoa yenu, mruhusu kwanza Yesu akufariji na kukuponya wewe binafsi. Anza kusoma kitabu cha Zaburi. Daudi alijua maana ya maumivu na kukataliwa. Na alijua msaada wake unatoka wapi. Soma na uone ni jinsi gani alimlilia Mungu na kumsifu Mungu hata katikati ya maumivu na mateso.

Kusifu ni njia yenyepo nguvu katika uponyaji. Huwezi ukamsifu Mungu kwa moyo wote na ukabaki na maumivu. Kwanza itafanyika kuwa dhabihu ya sifa (Waembrania 13:15), hutajisikia kujisifu. Lakini ukiweka nidhamu ya kuanza, utagundua kwamba unaingia katika uwepo wa Mungu na uponyaji wako kuanza.

Kudumu katika uwepo wa Yesu ni ufunguo wa uponyaji. Msifu Mungu kwa kutaja yeye ni nani na yale aliyoyatenda. Acha kuelekeza macho yako katika matatizo na matukio mabaya yanayokupata, bali mtazame Yesu. Jitahidi kumjua yeye zaidi ya hapo kwanza. Anza kuona kuwa hii ni fursa ya mwanzo inayokufanya umkaribie zaidi yeye.

Jambo muhimu lililotokea wakati nikisimama kuitetea ndoa yangu, nilimjua Yesu kwa namna ya kipee sana ambayo naamini nisingeipata kama nisingelazimishwa na matatizo yangu kumtegemea kabisa. Nilijua jinsi upendo wake ulivyo mkuu, uimara wake, moyo wake usiobadilika. Alifanyika ngome yangu wakati wa kimbunga changu. Hakuna mtu anayeweza kuninyang'anya upendo huo ambao tuluijenga wakati ule wa misukosuko yangu. Ninamjua Yesu kwa undani sana wakati huu wa amani kwa sababu nilimjua vizuri wakati wa mateso.

Mkaribie Yesu. Jitahidi kumjua yeeye kwa undani sana kuliko hapo mwanzo. Hebu uone wakati huu kama fursa na sio tatizo. Mruhusu Yesu akufariji na kukuponya. Yeye amekwisha kubeba mateso yako pale msalabani. Kwa sasa huhitaji kuyabeba mateso yako. Mpe yeeye na umruhusu afufuke ndani yako kwa nguvu yake ya uponyaji. *"Maana nitakurudishia afya, nami nitakuponya jeraha zako, asema BWANA, kwa sababu wamekuita, mwenye kutupwa, wakisema, Ni Sayuni, ambao hakuna autakaye"* (Yeremia 30:17)

Msifu Mungu kwa vile alivyo na kwa yale aliyoafanya. Mpe dhabihu ya sifa katikati ya maumivu yako na uponyaji utaanza kuonekana ndani yako. Pata muda wa kutosha wa kusoma neno la Mungu na mwombe Yesu aseme na wewe kupitia Neno lake. Anza kusoma kitabu cha Zaburi. Ona ni kwa jinsi gani Daudi alipata faraja na furaha ndani ya Bwana hata wakati wa mateso makali.

"Yesu unajua ninaumia. Hata wewe ulipata mateso maishani mwako. Ulipata maumivu ya kukataliwa, aibu na kushushwa. Uliyachukua na kuyapeleka msalabani kwa ajili yangu na sasa ninayaleta kwako. Ninakusifu Bwana! Ninalisifu jina lako! Nitatumia muda wangu kulisoma neno lako. Yesu, nifariji na kuniponya. Amina."

Msukumo

Uko katika mgongano wa ajabu. Hadi sasa umeamini kwamba mgongano wako ni kati yako na mwenzi wako. Siyo kweli. Ni mgongano kati ya falme mbili. Ni ufalme wa Shetani unafanya vita dhidi ya ule ufalme wa Mungu kwa mwenzi wako na ndoa yenu. Mungu ana mpango kwa ajili ya mwenzi wako. Ana mpango juu ya ndoa yenu. “*Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho*” (Yeremia 29:11).

Adui yako, yule mwovu, pia anayo mipango juu ya mwenzi wako. “*Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze*” (1 Petro 5:8).

Ni mpango wa Mungu kwamba mwenzi wako anageuka kabisa na ndoa yenu inarejeshwa na kuponywa. Ni mpango wa yule mwovu kwamba mwenzi wako apotee milele na kwamba ndoa yenu iharibike.

Mgongano ni rahisi. Mambo halisi ya mwenzi wako na hali ya unyumba wenu ni njia halisi ambazo yule mwovu ameamua kuzitumia katika shida yenu. Anajua mapungufu yenu ninyi nyote. Anajua ni nini kitakuumiza zaidi. Yule mwovu hana mchezo wa kirafiki. Bado atakukanyaga hata kama umeanguka chini. Unapojisikia mnyonge, yeye ndipo anakurushia mambo yale magumu. Lakini anakikomo katika njia zake za vita. “*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili*” (1 Wakorintho 10:13). Silaha za yule mwovu zina mipaka. Anaweza kuja kwako na silaha za kimwili – mambo ambayo ni ya kawaida kwa mtu. Hawezi kutumia silaha zenye uwezo wa kimaajabu ili kukushambulia. Mungu amekuahidi kwamba kuna njia ya kutokea katika kila shambulizi la yule mwovu.

Maandiko yana ahadi nyingi juu ya silaha zako. “*Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;) tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo*” (2 Wakorintho 10:3-5). Mungu amekupatia silaha zenye nguvu ya ajabu ili kupambana na yule mwovu.

Ufunguo ni kukaa katika roho na kuvipiga vita katika roho. Yule mwovu ni bwana wa mwili. Anaujua mwili wako zaidi ya vile unavyoujua wewe mwenyewe. Ukiwa mwilini, yeye atakushinda daima. Lakini ukidumu katika roho, utashinda daima.

Je! Ina maanisha nini kudumu katika roho? Tazama, mwenzi wako anasema na kufanya mambo yasiyopendeza mbele za Mungu. Lazima ukumbuke kwamba vita vyako si dhidi ya mwenzi wako. Soma Waefeso 6:12. Hupigani vita vya kimwili na damu. Mwenzi wako si adui yako, Shetani ndiye. Hivyo, kudumu katika roho ina maana kwamba utakapomsikia mwenzi wako anasema na kufanya mambo yasiyopendeza Mungu, usijibu kimwili. Kugomba kwa sauti ya juu, hila, majibishano na kutisha maana hizo zote ni njia za kimwili za kulisughulikia tatizo.

Gundua sasa hivi kwamba unavipiga vita dhidi ya ufalme wa kuzimu juu ya mwenzi wako na ndoa yako. Kudumu katika roho ina maanisha unavipiga vita vya kiroho dhidi ya adui yako wa kweli, yule mwovu, na sio kupigana katika mwili dhidi ya mwenzi wako. Mfikirie mwenzi wako ni kama mateka au mfungwa ndani ya kambi ya kijeshi. Vita vyako vya kiroho ndiyo itakuwa njia ya kumweka huru huyo mwenzi wako.

Matukio ndio silaha ya yule adui. Njia yake kuu ni kukufanya macho yako uyaelekeze kwenye matukio na siyo kwa Yesu. Je! Unasongwa na nini leo? Je! Mwenzi wako anataka talaka? Je! Mwenzi wako yuko kifungoni? Je! Unatishiwa usalama? Hajjalishi unakumbana na mambo gani, yote hayo ni matukio tu. Usiyaruhusu yakutawale. Bali, anza kubadilisha mwelekeo kwa njia ya maombi.

Sasa aina ya vita hii inakulazimu uione na kupata mafunuo ya kiroho. Haimaanishi kusema, "Mungu mpPENDWA wetu, ibariki ndoa yetu. Ahsante. Amina." Hii ina maanisha kuzitambua roho za kishetani zilizo kazini na kisha kuzichukua silaha za kiroho dhidi yake katika jina la Yesu. Ni vita vilivyo hai, siyo kukaa tu na kusubiri.

Si kusudi la kitabu hiki kukufundisha undani wa vita vya kiroho utakavyopambana navyo. Kuna vitabu vingi katika maduka ya Kikristo ambayo yatakufundisha juu ya kile unachokitaka kuhusiana na mada hiyo. Pia unaweza kumwuliza mchungaji wako akushauri ni kitabu gani kitakufaa.

Kusudi la kitabu hiki ni kukuimarisha kwa ajili ya vita iliyoko mbele yako. Kabla ya Yesu kupaa mbinguni aliwaambia wanafunzi wake kusubiri Yerusalem ili wabatizwa kwa Roho Mtakatifu (Matendo 1:4,5). Aliwaahidi kwamba watapokea nguvu baada ya tukio hilo (Matendo 1:8). Kwa wale aliowaambia tayari wamekwisha kuzaliwa mara ya pili alipowajilia baada ya kifo na ufufuo wake (Yohana 20:22). Ilikuwa dhahiri kulingana na kile kilichoandikwa katika Matendo ya Mitume kwamba Yesu aliwaahidi kutakuwa na uzoefu mwingine tofauti kabisa. Soma Matendo sura ya 1 na 2.

Je! Unayaona mabadiliko ya watu hao? Wale waliokuwa na hofu na hata kumkataa Yesu kuwa hawamjui, ghafla wanakuwa na ujasiri na kuitangaza injili bila hofu. Roho Mtakatifu aliposhuka kwa ishara za nguvu, aliuthibitisha uwepo wake kwa kuwapa ndimi mpya kila mmoja aliyeokuwa amemwamini.

Soma Warumi 8:26,27. Kama hatujui kuomba, Roho Mtakatifu anajua jinsi ya kuomba mapenzi kamili ya Mungu kupitia kwetu.

"Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda" (1 Wakorintho 14:14). Wakati huu wa misukosuko maishani mwako, unapaswa uweze kuomba akili zikiwa hazina matunda. Kutakuwa na watu wengi sana watakaokupa ushauri. Unapaswa kutambua ni nini Mungu anakisema katika kila hali. Njia pekee inayoweza kukusaidia kufanya hivyo ni Roho Mtakatifu kuomba mapenzi kamili ya Mungu kwa ajili yako na familia yako kulingana na kila hali inavyojitokeza.

Ukiwa unasoma kitabu cha Matendo ya Mitume, utaona kwamba ubatizo au kujazwa na Roho kulifanyika mara kwa mara. Haukuwa uzoefu wa mara moja tu katika historia ya kanisa au kwamba umetunzwa kwa ajili ya kundi fulani la watu wachache. Nguvu ile ile waliyokuwa nayo kanisa la kwanza unayo na wewe sasa. Unachopaswa kufanya ni kuomba (Luka 11:11-13).

Kama ni hitaji lako ya kwamba Roho Mtakatifu akujilie kwa nguvu sasa hivi, basi sali sala hii:

"Bwana Yesu nimekupokea wewe uwe Bwana na Mwokozi wangu. Ninazikataa kazi zote za yule mwovu ambazo zimekuwa sehemu ya maisha yangu. Nakuomba unibatize kwa Roho Mtakatifu."

Unaposali sala hii, subiri majibu ya Mungu. Mruhusu Roho Mtakatifu akujaze kwa wingi. Kwa muda mfupi maneno mapya yataanza kufanyika ndani yako. Kumbuka, maneno haya yatatoka katika roho na siyo katika akili zako. Usijisumbue kutaka kuyafahamu maana yake au kuyachambua. Wewe fungua kinywa chako na anza kumsifu Bwana. Iruhusu lugha ngeni aliyokupa kutumika wakati wa kusifu.

Unaweza kuitawala lugha hii mpya. Unaweza kuitumia wakati wa maombi ukitaka au kuacha kuitumia ukitaka pia. Siyo kwamba ni kitu ambacho kiko nje ya uongozi wako. Una itawala sawasawa tu kama ile lugha ya mama. Tofauti ni kwamba lugha ngeni ni lugha ya siri kati yako wewe na Mungu.

Pia unaweza kuimba kwa kutumia lugha hii ngeni. Chagua wimbo unaoupenda sana na anza kuuimba katika lugha hii mpya. Hutaelewa unasema nini, lakini Mungu ataelewa. Mwimbie, msifu yeye, mwombe yeye. Kadri unavyoitumia lugha hii mpya, ndivyo unavyozidi kuielewa zaidi. Usijali

hata kama hapo mwanzo ulipata neno moja au maneno mawili. Kadri unavyoyatumia maneno hayo, ndivyo maneno mengine yatakavyoongezeka.

Utagundua kuwa kuna mambo mengi tu ambayo yamekwisha kutukia tangu ujazwe na Roho. Maandiko Matakatifu yatakuingia kwa undani sana. Utaona kwamba una shauku kubwa ya kumsifu na kumwabudu Bwana. Utaanza kuimarisha uhusiano ulio imara na Roho Mtakatifu. Yeye ni mwalimu wako (Yohana 14:26) na mfariji wako (Yohana 16:7). Daima yeye humwinua Yesu, hivyo atakufundisha jinsi ya kumwinua yeye maishani mwako. Jifunze kuisikia sauti ya Roho Mtakatifu. Kwa maombi ya lugha mpya (kunena kwa lugha), atakuongoza katika mapenzi ya Mungu kwa kila hali maishani mwako.

“Bwana Yesu, ahsante kwa Roho Mtakatifu. Ahsante kwa mahusiano ya karibu ninapotembea nawe. Nisaidie kukumbuka kwamba vita vyangu si vya nyama na damu. Nisaidie nisighadhahibwe na matukio, yawe mabaya au mazuri, bali nikutazame wewe peke yako. Roho Mtakatifu, nifundishe, nishauri, nifariji. Ninajua unaomba mapenzi kamili ya Mungu kupitia kwangu ninaposali kwa lugha mpya uliyonipa. Nisaidie kuyatambua mapenzi ya Mungu katika kila hali maishani mwangu. Nifundishe jinsi ya kupigana vita vya kiroho dhidi ya adui yangu, yule mwovu. Amina.”

Maono Yasiyo Wazi

Kwa sasa unamtambua adui yako, hivyo mpende mwenzi wako kama Mungu anavyopenda, kwa pendo la agape, siyo pendo dhaifu la kibinadamu.

Warumi2:4 inasema ni wema wa Mungu unaotuongoza kuifikia toba. Mungu anatupenda katika ufalme wake. Tulipokuwa tungali wenyewe dhambi Kristo alikuwa kwa ajili yetu (Warumi 5:8). Mwenzi wako anapaswa kulijua pendo la Mungu lisilo na masharti. Haijalishi mwenzi wako anafanya nini, upendo wa Mungu haujabadilika.

Kama wewe ni mtu wa kujihesabia haki na kuwa na tabia ya kumhukumu mwenzi wako, utambue kwamba unachokionesha ni kwamba Mungu wako unayemwakilisha yuko hivyo. Kiburi cha jinsi hii hakitamfikisha mtu katika ufalme wa Mungu.

Dhambi yako ya kujihesabia haki mwenyewe siyo ndogo machoni pa Mungu kuliko ile dhambi "kubwa" ya mwenzi wako. Mungu haoni dhambi kubwa na ndogo. Mbele za Mungu dhambi ni dhambi. Nimewasikia watu wakiniambia kwamba wanawaombea wenzi wao ili wazaliwe mara ya pili na ndoa yao ipone na nimewatazama watu hao wakiwatumikisha wenzi wao kama takataka. Hiyo siyo njia ya Mungu na yeze hataheshimu tendo hilo la kumnyanyasa mwenzi wako. Kama umekuwa ukifanya hivyo, unapaswa utubu.

Unapaswa uharike kumsamehe mwenzi wako. Yawezekana hujisikii kufanya hivyo kwa sasa. Yawezekana hutajisikia kufanya hivyo kwa muda fulani. Hicho ndicho anachokutaka Mungu ukifanye—msamehe mwenzi wako. Hayo ndiyo mapenzi ya Mungu (Mathayo 6:14,15). Hebu linganisha mapenzi yako na yale ya Mungu na uwe tayari kumsamehe mwenzi wako. Uachilie moyo wako kwa Bwana na umruhusu yeze aanze kuubadilisha moyo wako. Hisia zitafuata baadaye. Usiziruhusu zitawale.

Anza kumwona mwenzi wako kama Mungu amwonavyo. Mungu ana mpango na kila mmoja wetu — **maono ya imani** anayoyatunza moyoni mwake akisubiri mtu akubaliane naye kwa ajili ya maono hayo. Ibrahim alipohiarika kulipokea neno la Mungu kuhusu mwanawewe na kuamini kulingana na mapenzi ya Mungu, ahadi ilitimia. Ahadi ya Mungu ilitimilika katika mwanawewe, Isaka.

Mungu ana mpango kwa ajili ya mwenzi wako. Mungu humwona mwenzi wako kwa macho yasiyo ya kibinadamu, na ndivyo Mungu anavyotaka umwone na wewe. Mungu anataka umwone mwenzi wako kwa mtazamo sahihi wa ki-Mungu.

Hadi sasa umekwisha kumwona mwenzi wako alivyo na kukubaliana na ukweli wa hali halisi. Hajakuwia vigumu kugundua kwamba mwenzi wako pamoja na ndoa yenu siyo ile iliyokusudiwa.

Yawezekana wewe mwenyewe umekuwa ukijiona katika mtazamo hasi. Yawezekana mawazo yako yamejawa na kumbukumbu ya mabaya yale uliyoyatenda au kuyasema ambayo ungependa yabadilike. Ni lazima uanze kujiona wewe mwenyewe, mwenzi wako, na ndoa yenu kama Mungu awaonavyo.

Wakati nilipokuwa nikisimama kwa ajili ya uponyaji wa ndoa yetu, nilikuwa najisikia vizuri tu kama Mikaeli hayupo nyumbani. Nilisoma Neno, niliomba katika roho, nilimsifu Mungu, na kuvipiga vita vya kiroho. Niliwaza na kuyalazimisha mawazo yangu kwamba kama Mikaeli atarudi nitamwonesha upendo wa Mungu usio na masharti. Sitagombana naye, sitakaa kimwili. Lakini mara Mikaeli alipoingia ndani baada tu ya kufungua mlango, ataniambia neno ovu na ugomvi kuanza mara moja. Kwa muda mfupi ataondoka tena huku akipaza sauti yake kwa kusema maneno kama vile,

"Wewe hutabadilika kamwe. Utabaki kuwa yuleyule. Unasema Yesu amefanya mabadiliko ndani ya maisha yako. Sawa, naku hakikishia siyaoni mabadiliko hayo."

Mara moja nitajutia maneno na matendo yangu na kutubu kwa kuwa katika mwili zaidi. Nilimwomba Mungu anisaidie ili niwe mzuri wakati mwingine (kama kweli kulikuwa na wakati mwingine) na baadaye nililia kwa muda wa masaa mawili hivi kwa sababu nilifikiri kwamba nimeuharibu mpango mzima wa uponywaji wa ndoa yangu.

Siku moja katika marudio ya mambo haya, Bwana alisema na moyo wangu. Akaniambia kwa nini nilimfanyia Mikaeli mambo kama hayo, sikumwonesha pendo la ki-Mungu lisilo na masharti, maana nilimwona kama alivyo na kumtendea yote hayo kwa sababu ya yale niliyoyaona. Mungu aliniambia kwamba neno lake halijafanyika ufunuo kwangu na nilikuwa nikilinukuu pasipo manufaa.

Soma Luka 4:1-13. Yule mwovu alipomjaribu Yesu, alimletea majaribu ambayo yatamaanisha kitu kwake. Yesu alikuwa na njaa baada ya mfungo wake mrefu, hivyo mkate lilikuwa jaribu lake sahihi. Yesu alikuja kuurejesha ufalme wa mbinguni, hilo nalo lilikuwa jaribu sahihi. Yesu aliuacha utukufu wake mbinguni akaja duniani kuwa mtumwa (Wafilipi 2:6-8). Pia jaribu la tatu lilikuwa sawa kwa kuwa lilikuwa ni changamoto kwa Yesu likintaka ajithibitishe kuwa yeze ni nani.

Kwa kujibu kila moja wapo ya hayo majaribu, Yesu alitumia Neno. Hakukubaliana na Shetani wala hakubishana naye. Badala yake alitumia neno kama upanga (Waefeso 6:17) na kupigana na Shetani katika ulimwengu wa roho. Kitu kilichomfanya Yesu afaulu sana katika majaribu haya ni kwamba yeze alilija neno la Mungu linasema nini juu ya kila moja wa hayo majaribu. Neno ndilo lilokua kipimo na alilitumia kama kipimo kwa kila jaribu.

Je! Unafahamu vile Mungu anavyomwona mwenzi wako? Siku ile Mungu aliponiambia kuwa Neno lake halijawa ufunuo kwangu, nilitambua kuwa alikuwa akiniambia kuwa sijamwona Mikaeli kama yeze amwonavyo. Nilimwambia anioneshe Mikaeli kutoka katika Neno lake ili nikubali.

Akanichukua hadi 1 Timotheo 3:2-4. "*Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu.*" Nilitubu mara baada ya kulisoma andiko hili kwa mara ya kwanza, sikuamini. Mume wangu alikuwa ni mlevi wa wanawake. Aliyadharau mambo ya Mungu na kunitania kwa ajili ya imani yangu. Niliisoma mistari hiyo tena na tena, "Bwana tunazungumza habari za mtu yule yule? Mungu akasema nami kitu cha kipekee sana ambacho natumaini utakielewa kwa mapana yake. Alisema, "Hivyo ndivyo nimwonavyo, Marilin. Yeze atakuwa mhubiri na mwalimu wa Neno. Wengi watakuja kwangu kuitia yeze. Unaweza kukubaliana na yule mwovu kuwa unamwona kwa macho yako ya kibinadamu au ukubaliane na Neno langu na kumwona kwa macho yasiyo ya kibinadamu."

Niliudhika. Mpaka hapo nimekuwa nikimsihi Mungu amvute Mikaeli aingie katika ufalme wake. Niliwaza kama ateweza kuingia kanisani au kuhudhuria semina ya neno la Mungu, angeweza kumwamini Yesu. Mawazoni mwangu daima nilimwona Mikaeli akifungua mlango kuingia ndani. Mara niligundua ni kiasi gani maono yangu yalikuwa chini sana kulinganisha na yale maono ya Mungu. Nilitubu na mara moja niliandika ile mistari nikiliweka jina la Mikaeli ndani ya andiko hilo. Nilianza kumwomba Mungu anioneshe mistari mingine ya Biblia ambayo inamhusu Mikaeli na nililiingiza jina la Mikaeli katika mistari yote niliyoipata. Ndipo Mungu akanionesha kitu kingine zaidi.

Alinipeleka katika Mwanzo sura ya 1, na kuniongoza katika habari yote ya uumbaji wa ulimwengu. Kisha akaniambia, "Kama mimi Mungu lazima niseme ili vitu viwepo na kupita, je! Ni kitu gani kinachokufanya uamini kwamba vitu unavyoviwaza vitafanyika?"

Niligundua kwamba wakati wa maombi andiko juu ya Mikaeli lilibaki kichwani mwangu. Nikaanza kuona kwamba kumbe ni muhimu yale maneno yaanze kusemwa hadharani ili ahadi itimie. Siku ile nilianza kuomba kwa kuisema ile mistari kwa sauti, "Mikaeli ni..." Wakati wa maombi niliyatamka yale maandiko kwa sauti na nilifanya hivyo kila mara niwapo katika maombi huku nikiwaza ni kwa kiasi gani Mungu anashughulika na Mikaeli huko aliko mahali fulani. Je! Atarudi nyumbani akiwa amebadilika?

Kisha kitu cha kuchekesha kilitokea. Siku moja Mikaeli alirudi kama kawaida yake na salaam ya maudhi. Ninakumbuka, nilikuwa nimesimama kwenye korido nikmtazama na niliwaza nafsini mwangu, "Ninashangaa kwa nini amesema hivyo. Huyu si yule wa mara zote." Punde si punde niligundua kwamba neno la Mungu limekuwa ufunuo kwangu. Mwanamume niliyemfahamu kutoka katika neno la Mungu alikuwa wazi kwangu zaidi ya yule aliyesimama kwangu kwa dharura akiwa amefungwa na yule mwovu. Niliwaza muda wote kuwa Mungu anapombadilisha Mikaeli, ananibadilisha mimi! Mungu alikuwa akishughulika nami ili nimwone Mikaeli kama alivyomwona ye.

Tangu wakati ule, hakuna kitu kilichobadilisha mtazamo wangu juu ya mume wangu. Niliweza kumpenda kwa pendo lisilo na masharti la agape kwa sababu nilijua kuwa ni wa thamani mbele za Kristo. Maneno na matendo yake yalikuwa wazi kwangu kuwa ni kazi ya yule mwovu. Aliposema, "Ninakuchukia na ninatamani nisingekutana na wewe." Hapo nilitambua ni kwa kiasi gani Shetani alinichukia. Kwa hakika haukuwa moyo wa yule mume ambaye atakuwa mhubiri wa injili na kufundisha katika jina la Bwana!

Kulikuwa na nyakati ngumu zaidi mbele yetu, lakini adui hakuweza kunitikisa baada ya kuzitambua zile ahadi za Mungu kwa Mikaeli. Haijalishi yule mwovu alinitupia maneno maovu kiasi gani, mimi nilinukuu, "Imeandikwa..." Neno la Mungu lilikuwa ufunuo kwangu.

Pia, liruhusu neno la Mungu lifanyike ufunuo kwako. Mwulize Mungu akuoneshe jinsi anavyomwona mwenzi wako. Yanukuu maandiko hayo na uyatamke kwa sauti kila siku. Acha imani ije kwa kusikia (Warumi 10:17). Kadri utakavyoyatamka, ndivyo utakavyoyasikia, na ndivyo utakavyomwamini Mungu kwa kile anachokisema.

Unapaswa kujiona wewe mwenyewe kama vile Mungu akuonavyo. Haijalishi umetenda mabaya gani huko nyuma, yalisamehewa ulipotubu. Usikubali yule mwovu akuambie kwamba wewe huwezi lo lote katika kuiponya ndoa yenu. Uponyaji wa ndoa yenu umesimama katika ukamilifu wa Yesu, siyo wako. Kile unachotakiwa kufanya ni kutii na kutubu pale unaposhindwa kutii. Hicho ndicho kitakachoyafanya mapenzi ya Mungu kupita katika nyumba yako. Mwombe Mungu akufunulie jinsi anavyokuona wewe. Liandike jina lako katika maandiko hayo. Yaseme maandiko hayo kwa sauti, yaruhusu masikio yako yasikie jinsi Mungu anavyomwona mtoto wake mpendwa – wewe!

"Bwana, ninakushukuru kwa Neno lako. Ninakushukuru kwa sababu wewe unalitunza Neno lako. Leo ninakubali jinsi unionavyo mimi pamoja na mwenzi wangu. Ninalikubali Neno lako juu ya ndoa na familia yetu. Sitaisikiliza sauti ya yule mwovu tena. Nitakubaliana na wewe tu. Liruhusu pendo lisilo na masharti, pendo la agape libubujike toka ndani yangu kwa ajili ya mwenzi wangu. Mruhusu _____ akuone wewe kuitia wema ninaouunesha katika jina lako. Amina"

Tiba ya Kimwili

Uponyaji utachukua muda. Unachotakiwa kufanya ni kumpa Mungu muda wa kutosha anaouhitaji ili kuitimiza kazi yote. Usiwe mwepesi wa kujikatia tamaa, fuata maelekezo yake na umruhusu akuponye kutokea ndani hadi nje.

Mpe muda wote anaouhitaji ili kushughulika na mwenzi wako. Usishikwe na msisimko na kujaribu kuyaharakisha mambo. Marko 4:26-29 inazungumzia juu ya mbengu ikuayo. Soma sasa hivi.

Tambua kwamba sasa unapanda mbengu za uponyaji wa ndoa yenu. Unapanda mbengu nzuri ili uvune mazao yaliyo mazuri. Wagalatia 6:7-9 inasema, “*Msidanganiyike, Mungu hadhiahikiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho.*”

Mungu ndiye mwenye majira ya hiyo mbengu uliyoipanda. Itafika wakati wa kuvuna itakapokuwa tayari imekomaa. Kila zao lina ratiba yake. Usiilinganishe ndoa yako na ndoa ya mtu mwengine. Usijaribu kuvuna mazao kabla hayajawa tayari. Usitake mambo yakae mahali pake kabla ya wakati. Mungu anajua itachukua muda gani hadi ndoa yako kuponywa. Yote yaache mikononi mwa Mungu.

Utapata marafiki na washauri wengi wazuri watakaojisikia kwamba umesubiri kwa muda mrefu. Watakwambia kwamba kama Mungu alikuwa na kitu cha kufanya, alipaswa awe amekifanya hadi sasa. Simama imara katika ahadi za Mungu. Mungu huitoa neema yake ya uvumilivu kwa yule anayepatwa na mateso na siyo kwa watazamaji. Kataika 2 Wakorintho 12:9, Bwana alisema na Mtume Paulo, “...*Neema yangu yakotosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu.*” Mungu hatakupa tu neema ya kupambana na yale yakupasayo, lakini ataikamilisha nguvu yake katika udhaifu wako.

Hebu uone muda huu wa uponyaji kama kozi ya uponyaji wa kimwili. Pale inapotokea mwili wa mwanadamu umeumia, huwa una tabia ya “kukakamaa” kadri unavyopona. Kazi ya mtaalam wa viungo vya mwili ni kuulazimisha mwili utembee hata kama mwili wenye haujisikii kufanya hivyo. Huwa kuna maumivu makali sana na mara zote si kile mgonjwa atapenda kufanya yeye mwenyeewe kama hana mtu wa kumlazimisha kufanya hayo mazoezi.

Ni kweli umeumizwa. Ndoa yako imeumizwa. Wakati mwengine inaonekana kuwa ni rahisi kukaa pale pale katika maumivu ukisubiri kwamba yatakwisha. Hata hivyo, Mungu ana mpango wa uponyaji, mpango huo utakusukuma kufanya hata yale ambayo kwa hiari yako usingewenza kuyafanya. Kwa wakati huu, si kwamba anaiponya ndoa yako tu, bali anakukuza ndani yako kwa kiwango ambacho yawezekana usingekifikia bila maumivu. Kwa wakati ambao utajisikia kwamba heri Mungu angekuacha tu na uendelee katika dhiki yako. Kama vile yule mtalaamu wa viuongo vya mwili wa mwanadamu, Mungu atakusaidia uende zaidi ya kile kikomo chako. Mpango wake ni kuleta utimilifu na afya katika ndoa yako ambavyo vitaleta utukufu kwake. Hafanyi yote haya kwa ajili yenu tu. Ana mwito juu ya maisha yenu ninyi nyote katika ndoa hii na ana mpango wa kugusa wengine kupitia ninyi.

Kama umesimama kwa ajili ya uponyaji wa ndoa yako ili kutimiza mahitaji yako, kuna muda utakuwa unafika ambapo unasahau kila kitu kinachotokea. Lakini kama utagundua kwamba kuna makusudi ya Mungu katika haya yote yanayotokea, utakuwa na nguvu na ujasiri wa kumruhusu Mungu kufanya kile anachotaka hata kama kinauma.

Muda uliotuchukua katika harakati za kuiponya ndoa yetu sasa unaonekana kuwa ni mfupi sana ukilinganisha na ile furaha ilijojengeka ndani yetu. Kwa hakika ameuponya muda na amekamilisha mengi ndani yetu na kupitia kwetu kwa miaka ambayo tumeplatana kuliko kama tusingempa miaka yote hiyo kwa ajili ya uponyaji. Tunda la miaka yote hiyo ya kusimama ni kubwa kuliko muda uliotuchukua.

Ni kweli kwamba leo Mikaeli ni mtauwa wa Bwana aliye msemaji miaka mingi iliyopita. Amezaliwa upya, amejazwa na Roho Mtakatifu na amewaka moto kwa ajili ya kazi ya Mungu. Yeye ni mhubiri na mwalimu wa neno la Mungu na amewavuta wengi kwa Bwana kama yeye Bwana alivyoahidi. Mungu ametutengeneza sisi wawili kwa ajili ya huduma ya ndoa na tumemwona Mungu akigusa maisha ya maelfu ya watu kupitia kwetu. Mungu ameipanua huduma yetu ulimwenguni kote ili wanandoa wa kila taifa na kila ulimi waweze kuutambua mpango wa Mungu kwa ajili ya nyumba zao. Ni upotevu wa namna gani kama tungemruhusu Shetani kuimiliki hii ndoa yetu.

Mungu ana mpango kwa ajili yenu ninyi wawili. Mungu amewapa kazi ambayo ni yenu peke yenu.

Ushindi uliopatikana nyumbani mwenu unaenda kuhudumu watu wengi kuliko ninyi mnavyoweza kufikiri.

“Bwana Yesu, ninakupa kibali cha kufanya kile upendavyo ndani yangu na maisha yangu. Ninajua kuna wakati ambapo mambo yatakuwa ni magumu, lakini ninakuruhusu unichukue zaidi ya kujisikia kuwa niko sawa. Nifinyange Bwana katika mfano wako. Nitumie Bwana kwa ajili ya utukufu wa jina lako. Baba ndoa yetu ikipatana na kupona, tutumie sisi kama mwili mmoja ili tulipeleke pendo lako na uponyaji wako kwa watu wengine. Naomba unipe maono kwa ajili ya mpango wako wa hapo baadaye. Katika jina la Yesu, Amina.”

NYUMA YA JALADA

Ndoa yao ilikuwa haina matumaini ya kupona kabisa, ilikuwa imevuka kiwango cha matengenezo kwamba hakuna mtu ambaye angeweza kuirejesha katika hali yake. Yesu ni yeye peke yake aliyeweza kuwapatanisha Mikaeli na Marilin Phillipps.

Mikaeli na Marilin waligundua kwamba uponyaji wa ndoa hautokei ndani ya usiku mmoja. Tabia zao na majeraha yao ya zamani yaliwfanya washindwe kuelewa kama mambo yangeweza kubadilika. Makovu ya mateso katika unyumba wao yamelichosha pendo lao na kuwaachia imani kidogo sana. Mazungumzo yalikuwa magumu na pendo la unyumba likiwa limeharibika kabisa. Ingawa, wote wawili waliendelea kukua polepole katika uhusiano wao na Bwana, uhusiano wao wenyewe ulikuwa umejaa maumivu na utupu wa kiroho.

Yesu alianza kuwathhibitishia wote wawili, Mikaeli na Marilin, kwamba pamoja na kuwaweka pamoja tena yeye atayaondoa maumivu na kuyaponya majeraha. Alianza kuwafundisha kanuni mbalimbali kutoka katika neno la Mungu ambazo zilisimamisha ndoa yao juu ya mwamba. Uponyaji ulipothibitika kwao, kanuni zile zile ziliwaimarisha na kuwakuza. Neno la Mungu liliyafanya yale ambayo wao wasingeweza kuyafanya pamoja na shauku yao ya kuwashirikisha wengine kanuni hizi za kiroho hali hii ilipelekea kuanzishwa kwa huduma ya Marriage Ministry International.

Kupitia huduma hii ya Marriage Ministry International, maelfu ya wanandoa watumishi wanahudumu kwa kuzitumia kanuni hizi kwa wanandoa wenzao. Kupitia upako wa Neno lake, Mungu anatengeneza nyumba za Kikristo ulimwenguni kote. Ndoa zenye majeraha zinaponywa na ndoa zenye afya zinapewa dira na makusudi ya kitauwa. Amri ya Marko 16:15-18 inatimizwa kwa njia nyingine yenye nguvu kwa wanandoa walio mwili mmoja wanapotiya moyo na kuimarishwa katika mwito wao na ule upako aliouweka ndani ya maisha yao kwa pamoja. Hailalishi ndoa yako ni nzuri au mbaya kiasi gani leo, Mungu ana mpango wa kitauwa kwa ajili yenu ninyi wawili.

